JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BODI YA KAHAWA TANZANIA

(Imeanzishwa kwa Sheria Namba 23 ya Mwaka 2001 na Marekebisho ya Sheria ya Bodi za Mazao ya Mwaka 2009)

TAARIFA KWA UMMA

YAHUSU TARATIBU MPYA ZA USIMAMIZI WA SEKTA YA KAHAWA

UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa maelekezo juu ya taratibu mpya za usimamizi wa sekta ya kahawa kuanzia msimu wa kahawa 2018/2019 unaotarajiwa kuanza mwezi wa Mei 2018. Maelekezo hayo yalitolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwenye kikao na viongozi wa Serikali kilichofanyika tarehe 14 Januari, 2018 mjini Dodoma. Maelekezo haya yanalenga kuboresha usimamizi wa sekta ya kahawa, kufufua ushirika na kuimarisha masoko ya kahawa ikiwa ni kutekeleza lengo la Serikali la kufufua mazao matano ya kimkakati mojawapo likiwa ni zao la kahawa.

Katika kutekeleza maelekezo haya Bodi ya Kahawa kama msimamizi wa sekta ya kahawa kwa mujibu wa Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kahawa 2013, inatoa mwongozo huu kwa wadau wa kahawa ili utaratibu huu mpya uweze kutekelezeka kama ilivyoelekezwa.

1. UZALISHAJI WA KAHAWA

Kwa kuwa asilimia 90 ya kahawa nchini inazalishwa na wakulima wadogo, ambao wanazalisha kwa tija ndogo inayosababishwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na miti ya kahawa yenye umri mkubwa, matumizi duni ya pembejeo, kutokuzingatia kanuni za kilimo bora, idadi ndogo ya miti kwa eneo, mashamba yaliyotelekezwa ambayo hayahudumiwi n.k. Bodi ya Kahawa itatoa mwogozo wa uzalishaji miche ya kahawa na mwongozo wa usimamizi wa kilimo cha kahawa. Miongozo hii itatumiwa na viongozi wa Serikali na wagani katika kusimamia utekelezaji wa maelekezo haya ya Serikali.

2. TARATIBU WA UTOAJI LESENI

Utaratibu wa utoaji wa leseni za kufanya shughuli mbalimbali katika sekta ya kahawa pamoja na usimamizi utabakia uleule kama ulivyoelekezwa katika kanuni za kahawa 2013.

3. SOKO LA SHAMBANI (FARMGATE MARKET)

Katika utaratibu huu mpya Serikali imeelekeza kuwa kuanzia msimu wa kahawa 2018/2019 unaotarajiwa kuanza Mei 2018, kahawa katika soko la awali itakusanywa kutoka kwa wakulima na vyama vya Msingi/AMCOS tu, ambavyo ndio vitakuwa na jukumu la kuipeleka kwenye viwanda vya kukobolea kahawa na baadae kwenye mnada wa kahawa. Wanunuzi wote wa kahawa (makampuni binafsi) watatakiwa kununua kahawa kwenye mnada wa kahawa ambao kwa sasa upo Moshi.

3.1. Utayarishaji wa kahawa ngazi ya awali

3.1.1. Utayarishaji wa kahawa laini za Arabika (Mild coffee processing)

Kuanzia msimu 2018/2019 wakulima watawajibika kutayarisha kahawa yao wenyewe kabla ya kuipeleka sokoni. Aidha majumbani mwao au kwenye viwanda vya kati vya kuchakatia kahawa (Central Processing Units (CPU) kupitia ushirika wao. Viwanda vya kati vya kuchakatia kahawa vitaendeshwa na wakulima wenyewe wakisimamiwa na wagani waliopo eneo husika.

- Viwanda vya CPU ambavyo ni vya wakulima na vilikodishwa na makampuni binafsi vitarejeshwa kwa wakulima na vitaendeshwa na wakulima wenyewe.

- Makampuni binafsi yanayomiliki CPU yawasiliane na uongozi wa Halmashauri za Wilaya na vijiji ambavyo CPU hizi zipo ili zikodishwe na zitoe huduma ya kuchakata kahawa za wanachama wa ushirika mpya wa wakulima utakaoanzishwa katika kijiji hicho.

Ni muhimu kuzingatia kuwa Serikali inataka viwanda hivi vya kati viendelee kufanya kazi na vitoe huduma kwa wakulima kwa makubaliano na ushirika wa wakulima. Bodi itakusanya fedha hizi za huduma za makampuni ambayo CPU zao zitakodishwa na kutoa huduma kwa wakulima.

3.1.2. Mitaji ya kuendeshea CPU

CPU kama kiwanda kidogo kinahitaji mtaji wa kugharamia shughuli za utayarishaji wa kahawa kabla ya kahawa kuwa tayari kupelekwa sokoni.Gharama hizo ni pamoja na mafuta/umeme wa kuendesha mashine, malipo ya wafanyakazi, ulinzi, bili ya maji n.k.

AMCOS ambazo zinamiliki CPU ziingie makubaliano na taasisi za fedha zinazoweza kuwapatia fedha za uendeshaji wa mitambo na usafirishaji wa kahawa kwenda kiwandani kwa ajili ya ukoboaji (secondary processing). Fedha hizi zitarudishwa/zitalipwa pindi mauzo ya kahawa ya AMCOS husika itakapouzwa mnadani. Ili kutekeleza suala hili kutahitajika makubaliano ya pande tatu ambazo ni AMCOS, Taasisi ya fedha na Bodi ya Kahawa. Serikali kupitia Afisa Ushirika ni lazima kuridhia kiasi cha fedha kinachohitajika kabla ya kukopa.

3.2. Utayarishaji wa kahawa Arabika ngumu na Robusta

Wakulima wanaotayarisha kahawa ngumu za Arabika na Robusta watatakiwa kufuata kanuni bora za utayarishaji wa kahawa ambazo ni kuvuna kahawa iliyoiva na baada ya mavuno kahawa huanikwa juu ya turubali/ mkeka au sakafu ya zege mpaka inapokauka na kuipeleka kwenye vyama vyao vya msingi.

4. UTAYARISHAJI KAHAWA NGAZI YA PILI (SECONDARY PROCESSING)

Viwanda vya kukoboa kahawa vitaendelea kutoa huduma ya kukoboa kahawa kwa vyama vya msingi kwa ushindani na kuzitayarisha kwa ajili ya kwenda mnadani. Aidha viwanda ndivyo vitatakiwa kuingia kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani (Warehouse Receipt System (WRS) ili kuwawezesha wakulima walioleta kahawa kupata fedha Benki wakisubiri mauzo ya kahawa zao minadani. Ushindani baina ya viwanda vya kukobolea kahawa unatakiwa kuwa katika maeneo ya gharama za ukoboaji, upatikanaji wa magunia, gharama za kuhifadhi, utoaji wa huduma nyingine kama usafiri n.k.

Viwanda vya ukoboaji vinashauriwa kutayarisha utaratibu wa kutoa huduma za usafiri wa kahawa kutoka vyama vya msingi/AMCOS hadi viwandani. Gharama hizo ambazo zitaridhiwa na Mrajisi pamoja na gharama nyingine za utayarishaji kahawa zitalipwa pindi kahawa za wakulima zitakapouzwa mnadani. Ili kuwezesha huduma hii kutakuwa na makubaliano ya pande tatu (AMCOS, Kiwanda na Bodi ya Kahawa) ambapo gharama hizi zitalipwa baada ya kahawa kuuzwa mnadani.

5. MASOKO YA KAHAWA

Kahawa zote zitauzwa kwa njia ya mnada. Utaratibu uliokuwepo wa kuwa na soko la moja kwa moja (direct export) umesitishwa.

5.1. Utaratibu mpya wa uendeshaji wa minada.

i. Wanunuzi wote wa kahawa kwenye mnada watatakiwa kuwa na cheti cha ulipaji wa kodi. (Tax clearance certificate)

ii. Wanunuzi mnadani watakaopata leseni pia watatakiwa kuweka kinga ya zabuni (*bid security)* katika akaunti ya Bodi ya Kahawa kuonyesha uwezo wa kulipia kahawa zao kwa wakati. Kiasi cha kinga hiyo kitakuwa katika makundi mawili; wanunuzi wakubwa (milioni 500) na wadogo (milioni 100). Kiasi hiki kinaweza kubadilika kuendana na hali ya masoko.

iii. Muda wa malipo ya kahawa iliyonunuliwa mnadani umepunguzwa kutoka siku saba hadi nne za kazi. (promptly date–4 days)

iv. Wauzaji mnadani wanatarajiwa kulipwa ndani ya siku saba za kazi baada ya mnunuzi kulipa.

v. Kutatayarishwa Katalogi ya kahawa spesheli ile ambayo itaingizwa kahawa zote zenye vyeti endelevu kama vile *Organic, Fair Trade, Rainforest Alliance, Café practices* na kahawa zenye alama za ubora zaidi ya 80 (80 cupping scores). Hili linaanzishwa ili iwe chachu kwa wakulima kuongeza ubora wa kahawa.

vi. Bei atakayolipwa mkulima itapatikana pale kahawa itakapouzwa mnadani na vyama vya ushirika vitalipwa ili vilipe wakulima fedha zao kulingana na kahawa waliyokusanya.

vii. Wauzaji kahawa mnadani hawataleta tena bei ya akiba (Reserve price). Dalali ndio atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuweka bei ya akiba kulingana na bei ya soko la kahawa.

viii. Vyama vikuu vya ushirika vitakavyoleta kahawa mnadani vinatakiwa kutokuchanganya kahawa hiyo kwa vyama tofauti ili kulinda ubora wa kahawa na bei ya vyama vitakavyoweka juhudi katika kuzingatia ubora wa kahawa na kahawa ya kila chama cha msingi itaonekana kwenye *catalogue Mf. KDCU – Kaisho RCS.*

ix. Bodi ya kahawa itatoa bei elekezi ya kahawa kwa vyama vya msingi na *union* zitakazofaa kulipwa kama malipo ya awali.

5.2. Masoko ya kahawa kwa wenye mashamba makubwa na wawekezaji

Wawekezaji wenye mashamba makubwa nao pia watatakiwa kuuza kahawa yao mnadani. Kwa wale ambao wana mikataba ya mauzo ya muda mrefu na wateja wao wa nje wataandaliwa utaratibu wao maalum na Bodi.

6. MFUKO WA MAENDELEO YA KAHAWA (TCDF)

Shughuli za Mfuko wa Wakfu wa Kahawa (Tanzania Coffee Development Trust Fund (TCDF) ulioanzishwa rasmi na wadau wa kahawa mwaka 2011 zimesimamishwa na shughuli hizo kuendelea kufanywa na Bodi ya Kahawa ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa miche kwa kutoa ruzuku ya miche ya kahawa kwa wazalishaji ili miche hiyo iweze kutolewa bure kwa wakulima, kugharamia mikutano ya wadau wa kahawa n.k

7. MAFUNZO KWA VYAMA VIPYA VYA USHIRIKA VYA KAHAWA

Ili kujenga uwezo wa vyama vipya vya ushirika kufanya na kusimamia biashara ya kahawa ya wanachama wao ipasavyo**,** Bodi ya Kahawa itatoa mafunzo ya ubora wa kahawa na masoko kwa vyama vyote vipya vya ushirika vitakavyoundwa kuanzia mwezi Machi, 2018 mara baada ya zoezi la kuunda vyama vya ushirika kukamilika.

8. MAFUNZO YA MASOKO YA USHIRIKI WA MNADA WA KAHAWA KWA MAKAMPUNI YALIYOKUWA YANANUNUA VIJIJINI

Bodi ya Kahawa itafanya mafunzo kwa makampuni yaliyokuwa yananunua kahawa vijijini ili kuyawezesha kushiriki na kununua kahawa kwenye mnada wa kahawa. Hili linafanyika ili kuongeza washiriki wa mnada na hivyo kuongeza ushindani na makampuni haya yaweze kuendelea na shughuli zao za biashara ya kahawa.

9. HITIMISHO

Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa zitaelekezwa kutengeneza sheria ndogo zitakazowezesha malengo yaliyoainishwa katika mwongozo huu kutekelezeka katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya.

Imetolewa na

KAIMU MKURUGENZI MKUU
BODI YA KAHAWA TANZANIA
S. L. P 732 MOSHI.